

Ofisi za Idara:

1700 - 155 Carlton St.
Winnipeg MB R3C 3H8
Nambari ya simu.
204-945-2476
Nambari ya simu isiyo na
malipo: 1-800-782-8403
Nambari ya kutuma Faxi:
204-945-6273
Anwani ya mtandao:
rtb@gov.mb.ca

143-340 9th Street
Brandon MB R7A 6C2
Nambari ya simu.
204-726-6230
Nambari ya simu isiyo na
malipo: 1-800-656-8481
Nambari ya kutuma Faxi:
204-726-6589
Anwani ya mtandao:
rtbbrandon@gov.mb.ca

113-59 Elizabeth Dr.
Thompson MB R8N 1X4
Nambari ya simu.
204-677-6496
Nambari ya simu isiyo na
malipo: 1-800-229-0639
Nambari ya kutuma Faxi:
204-677-6415
Anwani ya mtandao:
rtbthompson@gov.mb.ca

The Residential Tenancies Branch Idara ya Kupangisha Makaazi

MAMBO MAALUM

Idara ya Kupangisha Makaazi

Idara ya Kupangisha Makaazi ina majukumu manne:

- **Kupeana maelezo/Kujulisha**
- **Kuchunguza**
- **Kusuluhisha**
- **Kukata Kauli**

Kupeana Maelezo/Kujulisha

Tunapeana maelezo kwa wapangishaji na wapangaji kuhusu haki na majukumu katika *The Residential Tenancies Act* na *The Life Leases Act* na kuhusu kanuni zetu. Tunapeana maelezo kupitia kwa simu, ana kwa ana unapotutembelea au kwenye barua.

Tunapeana mafundisho kuhusu sheria yetu kwa vikundi vya wapangishaji , wapangaji au raia. Tunapeana masomo kujulisha watu kuhusu haki na majukumu ya wapangishaji na wapangaji.

Tuna makaratasi ya mambo muhimu kuhusu mada kadhaa kwa wapangishaji na wapangaji. Mada hizi zinazingatia: pesa ya stakabadhi, ilani, kupangisha chumba ulichopanga, haki ya kuingia, haki na majukumu.

Kuchunguza

Tunachunguza ikiwa sheria ya *The Residential Tenancies Act* na *The Life Leases Act* imevunjwa, na tunapeana maelezo zaidi ili kusaidia katika kutatua malalamishi. Maofisa wachunguzi huwasiliana na wapangishaji na wapangaji na mashahidi wowote au vikundi vya watu wowote wanaohusika (kwa mfano maafisa wa afya). Wapangishaji na wapangaji wana uhuru wa kupata ujumbe wowote tunaopata katika uchunguzi.

Kusuluhisha

Maofisa wetu hujaribu kusuluhisha mafaragano kati ya wapangishaji na wapangaji (kwa mfano kudai pesa ya stakabadhi, madai ya kurudishiwa pesa zozote, ilani ya kuhama). Ofisa msuluhishi hufanya kazi kwa pamoja na mpangishaji na mpangaji ili kuwasaidia kupata suluhisho litakolofurahisha kila mmoja. Suluhisho hutendeka kwa simu, kwa simu baadhi ya watu wengi kwenye mtandao, uso kwa uso au kwa barua/maandishi. Makubaliano kupitia kwa suluhisho yote hudhibitishwa kwa maandishi. Makubaliano yanaweza kuwekwa kwa sheria ikiwa kikundi kimoja kinakosa kuzingatia makubaliano.

(Pindua ukurasa)

Kukata Kauli

Kukata kauli kunahusisha utaratibu wa kuamua kesi. Kesi inaamuliwa wakati mwingine kupitia kwa kikao cha kusikiliza madai au kutokana na ujumbe uliopokelewa kwa maandishi kutoka kwa mpangishaji na mpangaji. Mpangishaji na mpangaji wanaweza kuhudhuria kikao cha kusikiliza kesi pamoja na ushahidi na mashahidi wao. Kila uamuzi hupeanwa kwa maandishi na maelezo kuhusu uamuzi hupeanwa. Kila uamuzi unaweza kukanushwa kwa kuweka rufani kwa Residential Tenancies Commission.